______________________________________________

______________________________________________

**4 Ulevi, Sherehe mbovu, na mambo kama hayo**

Burudani ni nzuri lakini, roho ya karamu na kutafuta raha huenda zaidi. Mara nyingi ni kidonge cha kuua maumivu tu. Inawaahidi watu njia ya kuepuka madhara katika maisha yao. Dawa za kulevya, pombe, televisheni, mtandao, na michezo ya video imekuwa njia maarufu za kutorokea.

**2 Timotheo 3:4** inatuonyesha mabadiliko ya vipaumbele kutoka kwa Mungu hadi furaha. Unaona nini katika aya hii inayowaelezea marafiki wako shuleni?

Angalia mifano hii miwili na uamue jinsi inavyokuathiri wewe.

**Roho ya kusherehekea**. Watu wamejaribu kuukwepa ukweli

na roho kwa karne nyingi. Soma Mithali 23:29-35 ili kugundua njia moja maarufu ambayo watu walijaribu kuepuka ukweli nyakati za Biblia.

Ni nini matokeo ya kujaribu kuepuka ukweli kwa namna hiyo?

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

Umeingizwa kwenye roho ya sherehe? Ikiwa ndivyo, unahitaji kufanya nini kuhusu hilo?

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

—> **Raha**.Tamaa kuu ya raha inajidhihirisha katika kununua. Tunapata nguo, magari, stereo, CD na maelfu ya mambo mengine. Mtu anayesisitiza sana kutafuta raha ni ili kudhibiti hali yake ya nje ili kuwa na furaha.

**Soma Mithali 21:17** ili kugundua kile kinachotokea tunapopenda raha kupita kiasi?

___________________________________________________________

___________________________________________________________

___________________________________________________________

Je, wewe ni mpenda raha? Ikiwa ndivyo, unahitaji kufanya nini

kuhusu hilo?

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

## KUVUA VIZUIZI VYAKO

Ni kikwazo gani kilichoorodheshwa hapo juu ambacho kinaingilia kati yako na uhusiano na Yesu Kristo?

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

**Soma Wagalatia 5:16-17.** Ni nini ufunguo wa kukitupa kikwazo hicho?

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

Katika sura ya mwisho, tulijifunza

jinsi ya kujazwa na Roho. Lakini 'tunaenendaje kwa Roho' kila siku

**kabla hatujakimbia mbio nzuri, sisi inatubidi kujifunza kuenenda kwa Roho**

**1 Mjazwe Roho Mtakatifu Daima (Waefeso 5:18)**
Tunapomwomba Roho Mtakatifu atujaze. Ataleta nuru eneo la

maisha yetu ambalo linahitaji kubadilishwa. Kuenenda katika Roho hufanyika tunapotoa eneo hilo kwa Bwana siku baada

ya siku. Tunaendelea kumruhusu Roho Mtakatifu atuangazie na kutubadilisha katika eneo hilo. Tunaweza kuomba daima. "Bwana. nijaze na unibadilishe."

**2 Usimzimishe Roho Mtakatifu (1 Wathesalonike 5:19)**
Je, inamaanisha nini "kumzima" Roho Mtakatifu? Kuzima maana yake ni kutupa maji juu ya moto. Tunatupa maji kwenye moto wa Roho Mtakatifu katika maisha yetu tunapochagua kutofanya yale anayotuelekeza kufanya. Kwa mfano, tunaposukumwa na Roho kumwita rafiki, lakini tusifanye hivyo, tumemzimisha Roho. Tunamzimisha Roho Mtakatifu tunapo chagua kutomtii. Ushawishi wake daima ni kwa manufaa yetu wenyewe, au wema wa wengine.

**3 Usimhuzunishe Roho Mtakatifu (Waefeso 4:30)**
Roho Mtakatifu huhuzunishwa kila tunapochagua kutenda dhambi kimakusudi. Kwa mfano, tunapojua kuwa si sawa kuchumbiana na mtu asiye mwamini, lakini tunachagua kufanya hivyo, tunamhuzunisha Roho. Kwa kufanya hivyo, tunasema ndiyo kwa kutenda dhambi na hapana kwa Mungu. Tunapofanya hivi, Roho Mtakatifu anasimama asitende lolote ndani mwetu na tunapoteza uwepo hai wa Mungu wa kuzungumza nasi, na kutuongoza.

## KUREJEA KWENYE NJIA SAWA

Tunafanya nini wakati tunajua hatutembei tena katika Roho? Hatujajazwa na Roho au tumemzima  au kumhuzunisha Roho? Tunarudi kwenye njia imara kwa kupumua kiroho. Kupumua kwa mwili huja kwa kawaida kwetu. Tumekuwa tukipumua wakati wote tumekuwa tukifanya kazi kwenye kikao hiki, lakini hata hatujawazia kupumua huko. Tunapumua nje, tukiondoa pumzi ya carbon dioksi kwenye mapafu yetu yote. Kisha

tunavuta pumzi ili kuchukua oksijeni inayotia uhai katika miili yetu.

Vivyo hivyo, kupumua kiroho huweka maisha yetu ya kiroho kuwa yenye afya. Baada ya kujizoesha kufanya mazoezi, itakuwa kama vile kupumua kwetu - kwa asili mchakato, inafanya kazi kwa njia isiyo ya kawaida tu. Tunatoa pumzi kwa kukiri. Kukiri maana yake tunakubaliana na Mungu. Tunaitambua dhambi maalum kisha tunakiri dhambi hiyo. Tunavuta pumzi kwa kumwomba Roho Mtakatifu atujaze (Waefeso
5:18). Jambo kuu la kupumua ni kwamba tunalifanya kila wakati. Ikiwa tutafanya kazi ngumu sana, kama kukimbia maili moja tunapumua zaidi kuliko kawaida. Upumuaji wa kiroho hufanya kazi kwa njia kama hiyo vilevile.

**Mungu anatupa sisi sote Roho Mtakatifu ili kukabiliana na mazingira yanayotukumba. Kwa kufanya hivyo, tunaishi ndani ya uwepo wa Mungu daima.**

**Kutembea** kwa Roho ni hatua kubwa unayoweza kuchukua kuelekea kupata sura mpya ya kiroho. Je,




unatembea kwenye Roho? Ili kufanya sehemu hii kuwa ya

kibinafsi katika maisha yako, fanyia kazi karatasi ya Mabadiliko ya Maisha kwenye "majaribu."

Rudia Wagalatia 5:19-21 na taja hasa baadhi ya vishawishi vinavyokuzuia kutembea pamoja na Roho.

**Kamilisha sehemu hii kwa kukariri Wagalatia 5:16.**

## KAZI

1. Kuwa na muda peke yako na Mungu kila siku wiki hii, kwa kutumia usomaji wa Biblia
ufuatao: Siku ya I: Marko
11:27-33

Siku ya 2: Marko 12:1-12

Siku ya 3: Marko 12:13-27

Siku ya 4: Marko 12:28-34

Siku ya 5: Marko 12:35-40

Siku ya 6: Marko 12:41-44

Siku ya 7: Marko 13

2. Kamilisha Kikao cha 9.

## MABADILIKO YA MAISHA

**Majaribu**

**Yakobo 1:2-4; 12-22**

Udhaifu wangu katika eneo la majaribu ni:

________________________________________________________________________

Nguvu zangu katika eneo la majaribu ni:

**Kitendo**

Kutokana na somo langu la Yakobo 1:2-4, 12-22, nina haja ya kumfanya Yesu kuwa Bwana juu ya majaribu yangu Kwa:

Nitachukua hatua mahususi ifuatayo ili kujitayarisha kushinda majaribu yo yote na kuenenda kwa Roho

**Waombezi Wenza**

Wataomba pamoja nami kuhusu hili

# SEHEMU YA 9




## Kubadilisha maisha yako

Na sasa kwamba twaelekea mwisho wa musimu wa michezo ya majaribio, naweza kutazama nyuma na kuona jinsi ambavyo nimekuwa bora. Ninahisi vyema japo ninaona haja ya kuendelea kujitahidi Zaidi. Sasa, lakufwatia ni lipi? Ni lini nitakapojua kwamba nimekwisha bobea, nimewasili?

Natumai umepitia hisia sawa za "Nini kifuatacho?" au "Ni lini nitajua nimefika?" Yesu amebadilisha maeneo mengi maishani mwako lakini unaweza kujiuliza, "Maisha yangu yanaendeleaje kubadilika?"

### HALI ILIYOBADILIKA

Ulipoamua kumfuata Yesu, mabadiliko makubwa yalitokea. Mengi yayo yalifanyika ndani yako. Mengi yayo hata hukuyajua kwamba yametendeka. Hukubadilishwa tu - ulipangwa upya kabisa!

**Soma Warumi 6:1-11**. Ni taswira gani inayoonekana ambayo Paulo anaitoa hapa? (Dokezo: ona mstari wa 3)

Eleza kile kinachotokea kwa mtu kimwili anapobatizwa.

______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________

Tengeneza orodha ya mabadiliko yanayotokea ndani yetu wakati "tunabatizwa" ndani ya Kristo?

______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________

Jifunze mchoro huu. Ni ukweli kukuhusu wewe kwamba u nani na jinsi Yesu alivyo kubadilisha maisha yako.

| **HALI ILIYOBADILIKA** | | |
|---|---|---|
| Kristo alikufa (6:3) | Kristo alizikwa (6:4) | Kristo alifufuka kutoka kwa wafu (6:4) |
| Ulipompokea Kristo, ulikufa | Ulipompokea Kristo, ulizikwa | Ulipompokea Kristo ulifufuka kutoka kwa wafu |

Rudia misemo ifuatayo tena na tena hadi uwe umeikariri

**Kristo alikufa, nami nilikufa. Kristo alifufuka, nami nilifufuka. Niko ndani ya Kristo. Kristo yu ndani yangu. Sasa nina kitambulisho kipya.**

Unaweza kusema, "Sijisikii kama kwamba nimekufa," au "Sijisikii kama kwamba ni hai!" Siku ya kwanza ya majira ya joto huenda usihisi jua linachoma ngozi yako. Lakini siku inayofuata unaweza kuona na kuhisi mabadiliko ambayo yamefanyika kwenye ngozi hiyo.

Hapa ndipo imani inapoingilia. Angalia jinsi Mtume Paulo anatupa hatua tatu za kutenda ili kuishi kile ambacho tumegundua katika Warumi 6:1-11.

"Jua" kile Mungu anasema juu yako (Warumi 4:6, 9). Anasema kuwa kwa sababu ya Kristo, utu wako wa kale (ubinafsi na dhambi)

umekufa na utu wako mpya (Kristo anayeishi ndani yako) u hai.

☐ "Jihesabu" kuwa umekufa kwa dhambi na u hai kwa Mungu (Warumi 6:11). Kwa sababu kile "unachojua" ni kweli, unaweza kukitegemea hakika kama vile 2 + 2 = 4, ahadi ya Mungu kwamba ulikufa na uko sasa hai pamoja na Kristo ni kweli. Itegemee!

☐ “Jitoe” kwa Mungu (Warumi 6:13, 14). Kwa sababu ya kile "unajua" na "kutegemea", unachagua kutojitolea kutenda dhambi lakini unajitoa kwa Mungu (chaguo za Mungu). Wewe utafanya maamuzi kama matokeo ya kile "unachojua" na unaweza "kukitegemea" kuhusu wewe ulivyo katika Kristo.

Hayo yote yanaweza kuonekana kuwa mapya na ya ajabu kwako. Lakini ndio msingi wa Injili, ni ukweli wa kiroho.

**Soma Warumi 5-8** tena na tena na uache ukweli huo uzame. Angalia Waefeso 2:1-6 ili kuona jinsi Paulo alivyoeleza wazo hilo sawa katika Waefeso.

| HALI ILIYOBADILIKA - 2 | |
|---|---|
| **kabla hatujawa waumini** | **Baada ya kuwa waumini** |
| Wafu katika makosa na dhambi (Waefeso 2:1) | Hai pamoja na Kristo (Waefeso 2:5) |
| Kukidhi matamanio yetu (Waefeso 2:3) | Alituinua na kutuketisha pamoja na Kristo mbinguni (Waefeso 2:6). |

## KUFIKIRI NA KUTENDA KULIKOBADILIKA

Je, "wewe mpya" ndani anakuwaje "wewe mpya" nje pia? Utu wa kale (ule, kabla hatujakuwa waamini), ulijifunza jinsi ya kufikiria na kutenda kwa njia fulani. Lakini mtu huyo mzee alikufa. Kwa kuwa tumekuwa sasa waamini na kupokea utu mpya, tunaanza kufikiri na kutenda tofauti. kivipi?

**Soma Wakolosai 3:1-4**, na ujaze maneno yanayokosekana.

| KUWAZA KULIKOBADILIKA | | |
|---|---|---|
| **Kristo aliinuliwa (3:1)** | **Kristo ameketi juu (3:1,2)** | **Kristo ataonekana (3:4)** |
| Ulikuwa___________ | Elekeza____________ | Utakuwa___________ |
| | Katika vitu | Pamoja naye katka |
| | | |

Sisi tunabadilika kiasi gani? Kabisa! **Kabisa! Kabisa!** Baada ya sisi kuwa 'mtu mpya' kwa sababu ya Yesu kuishi ndani mwetu, tutaanza kuona mabadiliko ya nje.

**Baada ya kusoma Waefeso 4:20-32**, fanya orodha ya mabadiliko ambayo Kristo anafanya ndani mwako.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

Andika kwa maneno yako mwenyewe jinsi unavyobadilika.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

Mabadiliko yetu ya nje yanategemea mawazo yetu ya ndani - kujifunza kufikiria kwa njia mpya. Nukuu hii inaturahisishia mchakato huo.

**Panda mawazo, vuna kitendo- Panda kitendo, vuna mazoea. Panda mazoea, vuna mtindo wa maisha. Panda mtindo wa maisha, vuna hatima!**

**Kwa maneno mengine, mawazo yetu huamua hatima yetu**

**A.W.Tozer alisema, "Jambo muhimu zaidi kukuhusu ni kile unacho fikiri kumhusu Yesu, kwa sababu kile unachofikiri juu ya Yesu ndicho kitakachoamua wewe ni nani na unaishi vipi."**

Unawezaje kupanda mawazo ambayo hatimaye yatavuna
hatima? Kuvua
na kuvaa.

**Soma Waefeso 4:20-24** na uweke mstari chini ya maneno “kuvua" na "kuvaa." Unavua nini na kuvaa nini?

**Kuvua**
Tunafanya mazoezi, tunatoka jasho. Tukitoka jasho, nguo zetu zinaanza kunuka. Ikiwa tutafanya kama zuzu, tutaendelea kuvaa nguo zetu za jasho kwa siku kadhaa hadi zinuke kabisa. Lakini ikiwa tutafanya kama mtu anayejiheshimu, tunavua nguo hizo, tunaoga, na kuvaa nguo safi.

Tunahitaji "kuvua" vitu vya kunuka kama vile tungeondoa mavazi machafu yanayonuka.

Soma Wakolosai 3:5-9. Ni nini baadhi ya mambo ya kunuka yanayostahili kuvuliwa?

Orodhesha vitu vya kunuka katika maisha yako kutoka kwenye orodha iliyo hapo juu. Kuwa mwaminifu.

Je, itakuwaje tukiamua kutoyavua mambo hayo? Fikiria wewe ni samaki na unaona mdudu mzuri kabisa anayening'inia majini. Unaogelea juu kumtazama mdudu. Mmmmm, unafikiri, anaonekana ni mzuri sana. Lakini ni bora nikae mbali. Nimeambiwa kwamba kwa

kawaida kuna ndoano iliyofungwa kwa
kamba ambayo imefungwa kwenye kijiti mwishoni mwa mdudu huyo.

Unaogelea mbali, lakini huwezi kumtoa mdudu huyo mkubwa, mnene na mwenye kuonekana mtamu kutoka akili yako.


Unaendelea kufikiria jinsi mdudu huyo angekuwa mtamu, kwa hivyo unaogelea nyuma na kumtazama tena. Unafikiri, hapana, anaonekana mzuri lakini bora nipite. Bado unaendelea kuogelea kumzunguka na kumzunguka tena – ukiangalia hali.

Kadiri unavyoogelea ndivyo mdudu huyo anavyoonekana mzuri zaidi. Unafikiri, naweza kumhisi tu anakwenda kwenye koo langu na jinsi atakavyopendeza. Hatimaye, chomp – unaangukia chambo, umenaswa, na wewe ni marehemu. Umekufa.

Yakobo 1: I3-15 inaeleza mchakato huo:

- ☐ Chimbuko la mawazo mabaya ( ndoano ya Shetani) -Yakobo 1:13
- ☐ Kivutio (mdudu) - Yakobo 1:14
- ☐ Mwanzilishi (samaki) - Yakobo 1:14
- ☐ Kushawishi (majaribu) - Yakobo 1:14
- ☐ Kuzaliwa kwa Dhambi (kuchukua chambo) - Yakobo 1:15
- ☐ Kukua kwa Dhambi (kunaswa) - Yakobo 1:15
- ☐ Kifo (chakula cha jioni leo) - Yakobo 1:15.

Mara tunapofikia hatua ya "Kuzaliwa kwa Dhambi", tunanaswa katika mzunguko kama huu:




Hatuwezi kudhibiti chanzo (Shetani). Wakati mwingine hatuwezi hata kukidhibiti kishawishi(chambo) anachotutupia. Lakini tunaweza kudhibiti mawazo yetu juu yake.

**Kulingana na Wakolosai 3:1-2**, tunayadhibiti vipi mawazo yetu?

Kwa nini hiyo inafanya kazi? (Wakolosai 3:3 )

**Kuvaa**

**Soma Wakolosai 3:12-17**. Nia zetu zinapofanywa upya, mabadiliko mema hutokea katika maisha yetu. Tengeneza orodha ya vitu ndani Ya kabati yetu kwa sababu Kristo anaishi ndani yetu.

**Kulingana na Wafilipi 4:8** tutavaa mambo haya wakati "tunapofikiri juu ya mambo haya." Tunahitaji kufikiria mambo ya aina gani

Tunawezaje kujifunza kufikiri juu ya mambo haya? Fuata mapendekezo matendaji haya.


1. *Jenga tabia ya kufikiria kwa uangalifu juu ya maisha yako katika Kristo*. Rudia hii kauli kila siku:

**Kristo alikufa, nami nilikufa. Kristo alifufuka, nami nilifufuka. Niko ndani ya Kristo. Kristo yu ndani yangu. Sasa nina kitambulisho kipya.**

2. *Kariri Maandiko*. Endelea kukariri Neno la Mungu. Itafanya upya akili yako. Rudia aya tulizozikariri. Zitakusaidia kuweka mawazo

yako juu ya "mambo ya juu."

3. *Pinga majaribu*. Majaribu yanatuzunguka pande zote. Lakini kwa sababu sisi ni viumbe wapya katika Kristo, tunaweza kupinga majaribu. Mungu atulinde.




**Kumbuka**: Uhai wako umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu (Wakolosai 3:3). Tunaweza kujifikiria kuwa tumelindwa dhidi ya majaribu ya nje na ndani. Tunapojaribiwa, tunakuwa na Yesu Kristo anayeishi ndani yetu tumekufa kwa dhambi (na wafu hawaitikii). Sisi tu hai kwa Kristo, kwa hiyo tunaweza kumwomba Yesu ashughulikie majaribu yoyote tunayokabiliana nayo.

Tukikubali na kutenda dhambi, tuna damu ya Yesu iliyomwagwa msalabani ili kutusamehe sisi dhambi zetu zote.

Kwa hivyo wazo fulani la dhambi linapokuja akilini, tunapoogopa, tunapojipata pweke, au kushinikizwa, FIKIRIA MAMBO HAYA!




Kuibinafsisha sehemu hii maalum kwa ajili yako, chagua eneo moja

la maisha yako (rejea katika orodha
kutoka Wakolosai 3:5-9 au Waefeso 4:25-32) na ufanye kazi kupitia karatasi ya Mabadiliko ya Maisha.

**Kamilisha sehemu hii kwa kukariri Wakolosai 3:1**

# KAZI

1. Kuwa na muda peke yako na Mungu kila siku wiki hii kwa kutumia

kufuatia usomaji wa Biblia.

Siku ya 1: Marko 14:1-2

Siku ya 2: Marko 14:3-9

Siku ya 3: Marko 14:10-1 1

Siku ya 4: Marko 14:12-16

Siku ya 5: Marko 14:17-21

Siku ya 6: Marko 14:22-26

Siku ya 7: Marko 14:27-31

2. Kamilisha sehemu ya 10.

## MABADILIKO YA MAISHA

**Mawazo na Matendo**
**Wakolosai 3:5-9 au Waefeso 4:25-32**
Udhaifu wangu na maisha yangu ya mawazo ni:

________________________________________
________________________________________
________________________________________

Nguvu zangu na maisha yangu ya mawazo ni:

________________________________________
________________________________________
________________________________________

**Kitendo**
Kutokana na somo langu la Wakolosai 3:5-9 au Waefeso 4:25-32,

ninahitaji kumfanya Yesu Bwana wa mawazo na matendo yangu kwa:

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

Nitachukua hatua mahususi ifuatayo ili kujiondoa katika dhambi hii ya mawazo na/au kitendo.

**Waombezi Wenza** __________________________________________
wataomba pamoja nami kuhusu hili.

**SEHEMU YA 10**




# Kufanya uchaguzi wako

Leo ndio iliyokuwa siku ya mwisho ya mchezo. Ninapotazama nyuma, inahimiza kuona jinsi nilivyoendelea kuwa bora. Kazi ngumu niliyoifanya imezalisha matunda. Baada ya mchezo huo, mmoja wa waelekezi aliniagiza ufadhili. Nimefurahi sana na kuhisi kuheshimiwa. Hiyo itaniongezea makali huku pia ikinipa changamoto ya kutosha!

Kumfanya Yesu kuwa Bwana hakukuhakikishii kwamba maisha yetu yanakuwa rahisi. Kwa kweli, changamoto huwa ngumu zaidi. Kadiri tunavyozidi kwenda pamoja na Kristo ndivyo shetani anavyotaka "kututoa nje." Lakini tuna ahadi tunaposonga mbele.

**Andika Wafilipi 4:19** kwa maneno yako mwenyewe.

Mathayo 13:44-46 inatoa mifano miwili inayoeleza nini maana ya kumfanya Yesu kuwa Bwana. Unaona ulinganifu gani kati ya mifano hii miwili na mfano wa mwanzo kuhusu kukubali udhamini?

**Kumfanya Yesu Bwana hufanya kazi hivi. Yesu anatupatia hundi isiyoandikwa chochote na kubadilishana na karatasi tupu.**

Hundi tupu ambayo Yesu anatupa inawakilisha kila kitu tunachohitaji ili kuwa na uzima ubora zaidi. Angalia mistari hii ili kugundua baadhi ya ahadi zilizojumuishwa katika "hundi tupu" ya Yesu.

Warumi 8:32

Waefeso1:3.

2 Petero1:3.

Kwa malipo ya hundi tupu, Yesu anatutaka tumpe maisha yetu kama karatasi tupu - bila mipaka. Anaweza kuandika juu yake matamanio yetu yoyote.

**Warumi 12:1-2** inaeleza jinsi mchakato unavyofanya

kazi. Neno la Paulo hapa ni "Kwa hiyo," kwa hiyo anarejelea kile alichokuwa akisema katika sura za awali za Warumi. (Wakati wowote tunaona "kwa hivyo" tunahitaji kuuliza "kwa hiyo" ni kwa ajili ya nini!). Anasema hivyo akizingatia uhusiano huu wa ajabu ambao tunao na Yesu, na kwa sababu ya kila kitu ambacho Yesu ametufanyia, tunapata "kutoa miili yetu kama dhabihu iliyo hai" Unafikiri hiyo inamaanisha nini?

Paulo anaposema "itoeni miili yenu," anamaanisha sisi tuweke kila tulicho - akili, hisia, tamaa, na uwezo wa kimwili - kwa Yesu. Yeye anamaanisha kwamba tunajitoa wenyewe kwa Mungu, kama vile dhabihu zilivyowekwa juu ya madhabahu katika hekalu la Kiyahudi. Mnyama
aliyekufa alitolewa kwa Mungu kama sadaka katika tendo la ibada. Hapa Paulo anasema tunapaswa kutoa miili yetu kama "dhabihu zilizo hai.

Tunaitoaje miili yetu madhabahuni?

- > Tunachagua kuweka maisha yetu madhabahuni kila siku. Tunachagua kila siku kufa kwaajili yetu.
- > Tunamwacha Mungu aondoe chochote kinachoshindana na matamanio yake Yesu kwetu sisi.
- > Pia Paulo anasema sisi ni dhabihu iliyo hai. Kristo anaishi ndani mwetu nasi tuko hai.

Je, tunapaswa kuwa "dhabihu iliyo hai" ya aina gani? (Warumi 12:1)

**Warumi 12:9-21** inatoa njia kadhaa za kuwasilisha miili yetu. Hizi ni kina nani?

Unafikiri jinsi gani Mungu anataka utoe mwili wako kama dhabihu iliyo hai?

**MAISHA YALIYOBADILISHWA**

Tunapofanya uamuzi wa kila siku wa "kutoa mwili wako kama dhabihu iliyo hai," basi tunaweza kuishi kila siku "juu ya madhabahu." Tunapojifunza kujiwazia sisi wenyewe kama dhabihu iliyo hai, tunajua kwamba Yesu anayeishi ndani yetu, anatubadilisha kila siku.

**Angalia Warumi 12:2** na ueleze jinsi mabadiliko haya yanatokea.

— "Msiifuatishe tena namna ya dunia hii" inatuambia kwamba tunaweza kupinga majaribu na kwamba tabia zetu za nje zitaweza kulingana na hamu yetu ya ndani ya kumpendeza Yesu wakati watu wanatushinikiza kufanya kitu kibaya.

— "Mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu." Huu ndio ufunguo

unaofungua mlango wa maisha yaliyobadilika. Ikiwa mawazo yetu hayafanyi mabadiliko, matendo yetu pia hayatabadilika.

— "Mtaweza kujaribu na kuthibitisha kuwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu ni mema kwetu, yanayopendeza, na mapenzi makamilifu." Tunapopokea hundi tupu ya ahadi kutoka kwa Yesu na kumpa karatasi tupu ya maisha yetu, basi tutajikuta katika mahali pazuri zaidi - katikati ya mapenzi ya Mungu! Uhusiano wetu na Mungu na maisha yetu hapa duniani husonga kutoka "nzuri," "kupendeza" hadi "kamilifu." Maisha yanaendelea kuwa bora na bora na bora!

**Unaonaje Warumi 12:2** ikifanya kazi katika maisha yako?

____________________________________________________
____________________________________________________
____________________________________________________
____________________________________________________
____________________________________________________

**Zawadi ya mungu**

**Angalia Warumi 8:28-29** ili kuleta pamoja yote ambayo tumegundua.

Je, mistari hiyo inasema nini?

____________________________________________________
____________________________________________________
____________________________________________________
____________________________________________________
____________________________________________________

Mistari hiyo inakuambia nini kuhusu wewe mwenyewe?

____________________________________________________
____________________________________________________
____________________________________________________
____________________________________________________
____________________________________________________

Mungu anaahidi kutumia kila hali katika maisha yetu kwa wema wakati sisi tunaitwa kwa kusudi lake. Kusudi lake ni kwa ajili yetu ili tufananishwe na mfano wa Mwanawe. Kwa maneno

mengine,
Mungu anataka tufanane naye katika kila nyanja ya maisha yetu.

Masuala ambayo tumefanyia kazi kwa kutumia karatasi za Mabadiliko ya Maisha yametusaidia kuzingatia baadhi ya masuala maalum katika maisha yetu ambayo yanahitaji kubadilika. Lakini hayo mabadiliko tayari yapo ndani mwetu, kwa sababu Roho Mtakatifu anaishi ndani yetu na anafanya mabadiliko hayo mara kwa mara.

Kwa mwanga wa wazo hilo, eleza kile **2 Wakorintho 3:18** inasema.

____________________________________________________
____________________________________________________
____________________________________________________
____________________________________________________
____________________________________________________
____________________________________________________

Sifa zinazofanana na Kristo zinazotokana na mabadiliko hayo ya ndani zitaanza kuonekane katika tabia zetu zaidi na zaidi tunapoendelea kumualika Yesu awe Bwana wa maisha yetu.

Je, umewahi kutunukiwa kombe? Kombe ni kitu maalum kwa mtu ambaye anaipokea kwa sababu inawakilisha mafanikio. Sisi ni kombe la Mungu. Anafanikisha kitu ndani yetu kwa kutufanya kuwa kama Yeye zaidi. Maisha Yetu yanaakisi Mungu kwa wengine. Watu wanapotuona, wao pia wanamwona Yesu.

Kombe ni la mtu ambaye jina lake liko juu yake, na mtu ataweza kufanya chochote anachotaka na kombe hilo lake. Wewe ni kombe lake Mungu. Anakumiliki wewe. Na ana kitu cha pekee sana anachotaka kukifanya na wewe!

Chukua dakika chache na uangalie nyuma juu ya wiki




kumi zilizopita ili kuona nini umegundua juu ya ubwana wa Yesu katika maisha yako na ni wapi Yesu amekuwa akifanya kazi ili kukubadilisha.
Nakili mawazo yako hapa.

______________________________________________________
______________________________________________________
______________________________________________________
______________________________________________________

Kagua karatasi za Mabadiliko ya Maisha kutoka kwa wiki tisa zilizopita. Jiulize:

Mungu amefanya nini kunibadilisha? Sasa angalia sehemu za Vitendo na uamue hatua yoyote zaidi ambayo Mungu anaweza kutaka uchukue kwa kila suala. Chagua suala na hatua ambayo ni muhimu zaidi ili Mungu afanye kazi kwenye maisha yako sasa hivi. (Tumia chati kwenye ukurasa wa 107 kurekodi majibu yako). Katika maombi, muulize Mungu kile ambacho anataka ufanye baadaye.

______________________________________________________
______________________________________________________
______________________________________________________
______________________________________________________
______________________________________________________
______________________________________________________

**Kamilisha sehemu hii kwa kukariri Warumi 12:1-2.**

Hundi tupu ambayo Yesu anatupa inawakilisha kila kitu tunachohitaji ili kuwa na uzima ubora zaidi. Angalia mistari hii ili kugundua baadhi ya ahadi zilizojumuishwa katika "hundi tupu" ya Yesu.

Warumi 8:32

_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________

Waefeso1:3

_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
____________________________________________

2 Petero1:3.

_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________

Kwa malipo ya hundi tupu, Yesu anatutaka tumpe maisha yetu kama karatasi tupu - bila mipaka. Anaweza kuandika juu yake matamanio yetu yoyote.

**Warumi 12:1-2** inaeleza jinsi mchakato unavyofanya kazi. Neno la Paulo hapa ni "Kwa hiyo," kwa hiyo anarejelea kile alichokuwa akisema katika sura za awali za Warumi. (Wakati wowote tunaona "kwa hivyo" tunahitaji kuuliza "kwa hiyo" ni kwa ajili ya nini!). Anasema hivyo akizingatia uhusiano huu wa ajabu ambao tunao na Yesu, na kwa sababu ya kila kitu ambacho Yesu ametufanyia, tunapata "kutoa miili yetu kama dhabihu iliyo hai" Unafikiri hiyo inamaanisha nini?

_______________________________________________
_______________________________________________

______________________________________________

Paulo anaposema “itoeni miili yenu,” anamaanisha sisi tuweke kila tulicho - akili, hisia, tamaa, na uwezo wa kimwili - kwa Yesu. Yeye anamaanisha kwamba tunajitoa wenyewe kwa Mungu, kama vile dhabihu zilivyowekwa juu ya madhabahu katika hekalu la Kiyahudi. Mnyama aliyekufa alitolewa kwa Mungu kama sadaka katika tendo la ibada. Hapa Paulo anasema tunapaswa kutoa miili yetu kama "dhabihu zilizo hai.

Tunaitoaje miili yetu madhabahuni?

- > Tunachagua kuweka maisha yetu madhabahuni kila siku. Tunachagua kila siku kufa kwaajili yetu.
- > Tunamwacha Mungu aondoe chochote kinachoshindana na matamanio yake Yesu kwetu sisi.
- > Pia Paulo anasema sisi ni dhabihu iliyo hai. Kristo anaishi ndani mwetu nasi tuko hai.

Je, tunapaswa kuwa “dhabihu iliyo hai” ya aina gani? (Warumi 12:1)

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

**Warumi 12:9-21** inatoa njia kadhaa za kuwasilisha miili yetu kwa Kristo. Wao ni kina nani?

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

Unafikiri jinsi gani Mungu anataka utoe mwili wako kama dhabihu iliyo hai?

_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________

MAISHA YALIYOBADILISHWA

Tunapofanya uamuzi wa kila siku wa "kutoa mwili wako kama dhabihu iliyo hai,"
basi tunaweza kuishi kila siku "juu ya madhabahu." Tunapojifunza kujiwazia sisi wenyewe kama dhabihu iliyo hai, tunajua kwamba Yesu anayeishi ndani yetu, anatubadilisha kila siku.

**Angalia Warumi 12:2** na ueleze jinsi mabadiliko haya yanatokea.
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________

— "Msiifuatishe tena namna ya dunia hii" inatuambia kwamba tunaweza kupinga majaribu na kwamba tabia zetu za nje zitaweza
kulingana na hamu yetu ya ndani ya kumpendeza Yesu wakati watu wanatushinikiza kufanya kitu kibaya.

— "Mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu." Huu ndio ufunguo unaofungua mlango wa maisha yaliyobadilika. Ikiwa mawazo yetu hayafanyi mabadiliko, matendo yetu pia hayatabadilika.

— "Mtaweza kujaribu na kuthibitisha kuwa mapenzi ya

Mwenyezi Mungu ni mema kwetu, yanayopendeza, na mapenzi makamilifu." Tunapopokea hundi tupu ya ahadi kutoka kwa Yesu na kumpa karatasi tupu ya maisha yetu, basi tutajikuta katika mahali pazuri zaidi - katikati ya mapenzi ya Mungu! Uhusiano wetu na Mungu na maisha yetu hapa duniani husonga kutoka "nzuri",  "kupendeza" hadi "kamilifu." Maisha yanaendelea kuwa bora na bora na bora!

**Unaonaje Warumi 12:2** ikifanya kazi katika maisha yako?

___________________________________________________
___________________________________________________
___________________________________________________
___________________________________________________
___________________________________________________

**Zawadi ya mungu**

**Angalia Warumi 8:28-29** ili kuleta pamoja yote ambayo tumegundua.

Je, mistari hiyo inasema nini?

___________________________________________________
___________________________________________________
___________________________________________________
___________________________________________________
___________________________________________________

Mistari hiyo inakuambia nini kuhusu wewe mwenyewe?

___________________________________________________
___________________________________________________
___________________________________________________
___________________________________________________
___________________________________________________

Mungu anaahidi kutumia kila hali katika maisha yetu kwa wema wakati sisi tunaitwa kwa kusudi lake. Kusudi lake ni kwa ajili yetu ili tufananishwe na mfano wa Mwanawe. Kwa

maneno mengine, Mungu anataka tufanane naye katika kila nyanja ya maisha yetu.
Masuala ambayo tumefanyia kazi kwa kutumia karatasi za Mabadiliko ya Maisha yametusaidia kuzingatia baadhi ya masuala maalum katika maisha yetu ambayo yanahitaji kubadilika. Lakini hayo mabadiliko tayari yapo ndani mwetu, kwa sababu Roho Mtakatifu anaishi ndani yetu na anafanya mabadiliko hayo mara kwa mara.

Kwa mwanga wa wazo hilo, eleza kile **2 Wakorintho 3:18** inasema.

______________________________________________________
______________________________________________________
______________________________________________________
______________________________________________________
______________________________________________________

Sifa zinazofanana na Kristo zinazotokana na mabadiliko hayo ya ndani zitaanza kuonekane katika tabia zetu zaidi na zaidi tunapoendelea kumualika Yesu awe Bwana wa maisha yetu.

Je, umewahi kutunukiwa kombe? Kombe ni kitu maalum kwa mtu ambaye anaipokea kwa sababu inawakilisha mafanikio. Sisi ni kombe la Mungu. Anafanikisha kitu ndani yetu kwa kutufanya kuwa kama Yeye zaidi. Maisha Yetu yanaakisi Mungu kwa wengine. Watu wanapotuona, wao pia wanamwona Yesu.

Kombe ni la mtu ambaye jina lake liko juu yake, na mtu ataweza kufanya chochote anachotaka na kombe hilo lake. Wewe ni kombe lake Mungu. Anakumiliki wewe. Na ana kitu cha pekee sana anachotaka kukifanya na wewe!




Chukua dakika chache na uangalie nyuma juu ya wiki kumi zilizopita

ili kuona nini umegundua juu ya ubwana wa Yesu katika maisha yako na ni wapi Yesu amekuwa akifanya kazi ili kukubadilisha. Nakili mawazo yako hapa.

_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________

Kagua karatasi za Mabadiliko ya Maisha kutoka kwa wiki tisa zilizopita. Jiulize:
Mungu tayari amefanya nini kunibadilisha? Sasa angalia sehemu za Vitendo na uamue hatua yoyote zaidi ambayo Mungu anaweza kutaka uchukue kwa kila suala. Chagua suala na hatua ambayo ni muhimu zaidi ili Mungu afanye kazi kwenye maisha yako sasa hivi. (Tumia chati kwenye ukurasa wa 107 kunakili majibu yako).
Katika maombi, muulize Mungu kile ambacho anataka ufanye baadaye.
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________

**Kamilisha sehemu hii kwa kukariri Warumi 12:1-2.**

## KAZI

I. Kuwa na wakati peke yako na Mungu kila siku wiki hii, kwa kutumia
kufuatia usomaji wa Biblia.

Siku ya I: Marko 14:32-42

Siku ya 2: Marko 14:43-65

Siku ya 3: Marko 14:66-72

Siku ya 4: Marko 15:1-15

Siku ya 5: Marko 15:16-47

Siku ya 6: Marko 16:1-14

Siku ya 7: Marko 16:15-20.

**MABADILIKO YA MAISHA**

Kitabu kinachofuata katika mfululizo wa vitabu vya Hatua kuelekea Ukomavu, *Kuishiriki Imani Yako*, kitakusaidia kujifunza jinsi ya kuwasiliana kuhusu maisha ya Yesu Kristo kwa wengine. kiagize kutoka kwa www.reach-out.org au piga simu 1-800-473-9456.

| Mada | Kile Ambacho Mungu Amefanya Tayari | Kile Mungu Ananiongoza Kutenda Sasa |
|---|---|---|
| **Ukwasi wa Mali** | | |
| **Uchumba na Ngono** | | |
| **Urafiki** | | |
| **Wazazi** | | |
| **Mitazamo** | | |
| **Mazoea** | | |
| **Majaribu** | | |
| **Maisha yaliyowaziwa** | | |

# JINSI YA KUSOMA MAANDIKO

**TAZAMA** (Tumia karatasi kwenye sehemu ya Kichwa na Mstari Mkuu wa Jibu lako la Biblia)
Omba Roho Mtakatifu aseme nawe, kisha usome kifungu mara
kadhaa. Soma kwa akili iliyo wazi, tayari kupokea
na kutii kile ambacho Mungu anachokufundisha.

**FAFANUA** (Tumia sehemu ya Muhtasari ya karatasi yako ya Majibu ya Biblia.)
Hatua ya I - Soma mistari kabla na baada ya kifungu ili kuelewa mazingira na muktadha wake.

**Hatua ya 2 -** Jiulize maswali haya kuhusu kifungu: Nani? Nini? Lini? Wapi? Kwa nini? Vipi? Kisha andika ufahamu wako katika muhtasari.
**Hatua ya 3 -** Tafuta maneno usiyoyafahamu katika kamusi au kamusi ya Biblia.
**TEKELEZA** (Tumia pamoja na karatasi kwenye sehemu ya Matumizi Binafsi ya Jibu lako la Biblia)

**Hatua ya 1 -** Tafuta:

| | |
|---|---|
| —Ahadi za kudai | — Amri za kutii |
| —Mitazamo ya kubadilisha | — Hatua za kutenda |
| —Changamoto za kukubali | —Mifano ya kufuata |
| —Dhambi za kuungama | — Ujuzi wa kujifunza |

**Hatua ya 2 -** Eleza jinsi kifungu kinatumika kwako kwa kujiuliza maswali haya: "Ninawezaje kufanya kifungu hiki kuwa changu binafsi?" “Nawezaje kuifanya kwa vitendo?" "Ninawezaje kuifanya iweze kupimika?" Kuwa mahususi.

**KARIRI**

Tafuta mstari au kifungu cha Maandiko ambacho kinazungumza nawe kibinafsi, na ukikariri. Wakati wa mfululizo wa vitabu vya *Hatua Kuelekea Ukomavu*, zingatia kukariri mistari kama unavyopewa. Utapata hatua maalum za Kumbukumbu ya Maandiko kwenye ukurasa wa 101 wa *Kutumia Muda Peke Yako na Mungu*.

## MISTARI YA BIBLIA YA KUKARIRI

Kila mstari wa kumbukumbu kwenye kadi hizi umechapishwa katika toleo la New International (NIV). Mistari hiyo inalingana na sehemu mbalimbali katika kitabu hiki.

## TEMBEA NA MISTARI HII POPOTE UENDAPO

Tumia kile kinachokusaidia zaidi:

—Zungusha mpira kwenye kadi hizo.

—Zibebe kwenye bahasha.

—Ziweke kwenye pochi lako au kijitabu cha mfuko.

—Ziweke kwenye gari lako.

—Zibebe katika Biblia yako.

—Kila siku pitia kila mstari ambao umejifunza.

—Muambie mtu aangalie maendeleo yako kila wiki.

—Tumia kila mstari katika maisha yako ya kila siku.

| | |
|---|---|
| **1. KUMTAFUTA MUNGU**<br>**Zaburi 63:1**<br>1 Ee MUNGU, Mungu wangu, nitakutafuta mapema, Nafsi yangu inakuonea kiu, Mwili wangu wakuonea shauku, Katika nchi kame na uchovu, isiyo na maji (NIV). | **6. MITAZAMO**<br>**Wafilipi 2:5**<br>Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu (NIV) |
| **2. GHARAMA YA UANAFUNZI**<br>**Mathayo 16:24**<br>Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi wake, Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate. (NIV) | **7. ROHO MTAKATIFU**<br>**Waefeso 5:18**<br>Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho; (NIV). |
| **3. UTAKATIFU**<br>**1 Petro 1:15-16**<br>bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote; kwa maana imeandikwa, Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu. (NIV). | **8. ISHI KWA ROHO**<br>**Wagalatia 5:16**<br>Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili (NIV). |
| **4. IMANI**<br>**Waebrania 11: 1**<br>Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana (NIV). | **9. FIKIRIA**<br>**Wakolosai 3:1**<br>Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. (NIV). |
| **5. UTIIFU**<br>**Yohana 14:21**<br>Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake. (NIV). | **10. DHABIHU ILIYO HAI**<br>**Warumi 12:1-2**<br>Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu. (NIV) |